**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2026**
**Dodoma**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule 0759843430/0685784780**
**Makamu Mkuu wa Shule 0753225444/0786489450**
**Matron 0620176923/0757500686**

**SHULE YA SEKONDARI MANGA**
**S.L.P 305**
**TARIME-MARA**
**…………………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

**YAH:MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MANGA HALMASHAURI YAWILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA MWAKA ...................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Manga ipo umbali wa Kilometa 04 kutoka barabara kuu itokayo Mwanza kwenda Sirari.Wanafunzi wanaotoka mikoa jirani tofauti na mkoa wa Mara wa kifika Mwanza waende stendi ya Nyamhongoro wapande magari yaendayo Tarime au Sirari washuke kituo kidogo kitwacho Gachuma/ Komaswa. Hapo wachukue pikipiki nauli ni Tsh. 3,000/= hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ................., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe .................. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………... Wanafunzi watapokelewa jumatatu hadi ijumaa kuanzia saa 2:00 asubuhi hada saa 11:30 jioni. **Kamwe** hakuna mwanafunzi atakayepokelewa **jumamosi** na **jumapili.**
**Aidha** mwanao akichelewa atakosa vipindi vitakavyofundishwa kuanzia tarehe ya kuripoti hivyo ni muhimu kuwahi kuripoti shuleni.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -**

**2.1. Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili rangi ya idara ya maji rinda box kitambaa kizito na iwe ndefu kufikia vifundo vya miguu**.** Ili kuepusha mkanganyiko wa rangi na mishono tofauti. Sketi zitapatikana shuleni kwa Tsh.25,000/= kwa kila sketi kwa mlezi/mzazi atakayependa
ii. Shati 02 nyeupe ya mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni Raba nyeupe.
v. track suit ya light blue ikiwa na tshirt yake rangi sawa na track suit.
vi. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
vii. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu.
viii. Track suit rangi ya Kijivu kwa ajili ya masomo ya usiku (prepation time) ikiwa na tshirt yake rangi sawa na track suit.
ix. Aje na Sweta rangi ya dark blue (V-shaped) iliyo na michirizi meupe shingoni na mikononi. Kwa mzazi/mlezi atakayependa zinapatikana shuleni kwa Tsh.20,000/= kwa moja.
x. Mwanafunzi aje na nguo za kushindia /kuvaa wakati wa shughuli za nje (shamba dress) ni magauni mawili rangi ya pinki rose mshono wa solo ndefu hadi chini. Kwa mzazi/mlezi atakayependa zinapatikana shuleni kwa Tsh.30,000/= kwa kila gauni.
xi. Mwanafunzi aje na Tsheti 02 rangi ya dark blue yenye kola ya "cream". Kwa mzazi/,lezi atakayependa zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh.15,000/= kwa kila moja.

**MUHIMU:**

**a) mwanafunzi anatakiwa kuwa na pea mbili kwa kila sare iliyoandikwa hapa.**
**b) Wakati wa kuripoti mwanafunzi aje akiwa amevaa track suit na sio nguo za nyumbani.**

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari, Kaunta book nane na kalamu za kutosha rula moja na mathematical set.
ii. **Ream 04 (Double A)** kwa mwaka,ream za kawaida hazitapokelewa.
iii. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika (Combination) mfano kwa shule hii ni **CBG**, **PCB, HGK** na **HGL**

| S/N | SOMO | AINA YA KITABU |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | BIOLOGY | 1. BIOLOGY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE (Tanzania Institute of Education)<br>2. BIOLOGY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM SIX (Tanzania Institute of Education) |
| 2. | CHEMISTRY | 1. GENERAL AND INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE & SIX (Tanzania Institute of Education)<br>2. ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE & SIX (Tanzania Institute of Education)<br>3. PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE & SIX (Tanzania Institute of Education) |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | GEOGRAPHY | 1. PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE & SIX (Tanzania Institute of Education)<br>2. PHYSICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE & SIX (Tanzania Institute of Education) |
| 4. | PHYSICS | 1. PHYSICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE (Tanzania Institute of Education)<br>2. GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM SIX (Tanzania Institute of Education) |
| 5. | HISTORY | 3. HISTORY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE (Tanzania Institute of Education)<br>4. HISTORY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM SIX (Tanzania Institute of Education) |
| 6. | KISWAHILI | 1. KISWAHILI LUGHA NA SARUFI KIDATO CHA TANO (Taasisi ya Elimu Tanzania)<br>2. KISWAHILI KIDATO CHA SITA (Taasisi ya Elimu Tanzania) |
| 7. | ENGLISH LANGUAGE | 1. ENGLISH FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE (Tanzania Institute of Education)<br>2. ENGLISH FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM SIX (Tanzania Institute of Education) |
| 8. | HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI | 1. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI KIDATO CHA TANO (Taasisi ya Elimu Tanzania)<br>2. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI KIDATO CHA SITA (Taasisi ya Elimu Tanzania) |
| 9. | ACADEMIC COMMUNICATION | 1. ACADEMIC COMMUNICATION FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM FIVE (Tanzania Institute of Education) |

| | | |
|---|---|---|
| | | 2. ACADEMIC COMMUNICATION FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENT'S BOOK FORM SIX (Tanzania Institute of Education) |

**<u>MUHIMU:</u>** Mzazi/mlezi unashauriwa umnunulie mwanao vitabu vilivyoorodheshwa kulingana na tahasusi aliyochaguliwa kwani vitabu hivyo vitakaguliwa siku ya kuripoti shuleni.

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma somo la Biology;
v. Scientific Calculator fx991 Kwa masomo ya Physics, Chemistry, kwa wanafunzi wote.(zitapatikana shuleni kwa tsh 35,000/=) kwa mzazi/mlezi atakayependa
vi. Golves box moja lenye PC 100 kwa tahasusi ya PCB na CBG
vii. Godoro la futi tatu.
viii. Mashuka Shuka pea mbili, pea moja ya light blue na pea moja ya pink na foronya zake Jozi 2, blanket 1, chandarua 1
ix. Blanket 1
x. Chandarua 1
xi. Nguo za ndani za kutosha; tauro moja, kanga pea moja ya kuogea ,pedi pakti 06 na night dress.
xii. File moja la kutunzia kumbukumbu zake ofisini (aina ya spring file) ambalo itapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh.2,000/=
xiii. Vyombo vya chakula na maji ya kunywa (sahani, bakuli, kijiko, kikombe kidumu cha lita 5 kwa ajili ya kutunza maji ya kunywa);
xiv. Ndoo 2 ( ndogo lita Kumi na kubwa lita ishirini 1) zenye mifuniko;
xv. Kiwi, dawa ya meno, mswaki na brush.
xvi. Dawa ya chooni lita 5 aina ya dexi inapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh. 12,000/= kwa mzazi atakayependa
xvii. Dawa ya mbu (RUNGU) kubwa
xviii. Kama ni mgonjwa aje na cheti cha Daktari.
xix. Wanafunzi wote wanaosoma mchepuo wa PCB na CBG wanatakiwa kuja na koti la laboratory rangi nyeupe(mikono mirefu) na urefu wa koti uwe usawa wa goti kwa ajili ya kuzuia madhara ya kemikali wakiwa maabara kwenye masomo ya vitendo.
xx. Mask (barakoa) box moja lenye PC 100 kwa mchepuo wa PCB na CBG.

## VIFAA VYA USAFI

| TAHASUSI | VIFAA ATAKAVYOLETA |
|---|---|
| PCB | Fyekeo,jembe na mpini, dawa ya chooni aina ya dexi, soft broom 01,reki, toilet brush na Squizer. |
| CBG | Squizer,jembe na mpini,reki na dawa ya chooni aina ya dexi,soft broom 01 na toilet brush |

| | |
|---|---|
| HGK | Fyekeo, jembe na mpini, mfagio wa nje 01, dawa ya chooni aina ya dexi , hard broom 01, mooper na reki. |
| HGL | Fyekeo,jembe na mpini, reki, dawa ya chooni aina ya dexi, soft broom 01,hard broom, mooper, na Squizer. |

## 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo kwa sare za darasani tu | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

3 Michango hii iliyoorodheshwa hapo juu (**Tsh 80,000**) ilipwe kwenye akaunti namba **30401200103 NMB BANK** jina la akaunti **MANGA SECONDARY SCHOOL**. Mwanafunzi aje na pay in slip iliyoandikwa majina kamili ya mwanafunzi na aiwasilishe wakati wa usajili.

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayonipamojana;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kuhama bweni.**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum kutoka kwa Mkuu wa Shule ikiwa kama ni mgonjwa au kwa sababu za msiba.**
- ❖ **BIMA YA AFYA. mwanafunzi aje na bima yake ya afya kwa matumizi yake. Ili kuepusha gharama za matibabu. Ni muhimu aje nayo siku anaporipoti shuleni.**

## 3.2 Makosa yatakayo sababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wakaribu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu ili mwanao aweze kupata elimu bora.***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MANGA***

Wako,



**EDITHA L. NAKEI**
**MKUU WA SHULE**

HEADMISTRESS
MANGA SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 305
TARIME.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na kuwaomba watume fedha+. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **mkuu wa shule ;- 0759843430/0685784780**
- **makamu mkuu wa shule ;- 0753225444/0786489450**
- **Matron 0620176923/0757500686**
- **Mtaluma Mwandamizi 0759-752032**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI MANGA**
**HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI**

1. JINA LA UKOO………………………………………………JINA LA KWANZA…………………………………………………….
   JINA LA KATI……………………………………………………………….
2. JINA LA MZAZI / MLEZI……………………………………………………………………………………………………………
3. KAMA NI MLEZI: UHUSIANO…………………………………………………NAMBA YA SIMU……………………………
4. ANUANI YA KUDUMU YA MZAZI/MLEZI…………………………………………………
5. TAREHE YA KUZALIWA ………………………………………………
6. MAHALI MWANAFUNZI ALIPOZALIWA:- KIJIJI CHA ……………………………KATA YA……………………………..
   WALAYA YA ……………………………MKOA WA …………………………………
7. DINI…………………………………………………………………..DHEHEBU………………………………………………..
8. UNAINGIA KIDATO CHA ……………………………….TAREHE /MWAKA………………………………………
9. KUTOKA SHULE YA MSINGI………………………..WILAYA YA …………………………..MKOA WA ………………
10. MZAZI/MLEZI WAKO ANAFANYA KAZI YA AJIRA/MKULIMA/BIASHARA…………………………………………
11. NDUGU WENGINE AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA HABARI NUHIMU JUU YAKO.
    i. JINA……………………………………………………..UHUSIANO……………………NO. SIMU……………………
    ii. JINA……………………………………………………..UHUSIANO……………………..NO.SIMU……………………
    iii. JINA……………………………………………………..UHUSIANO……………………..NO.SIMU……………………
12. SIFA MAALUMU KAMA UNAZO………………………………………………………………………………………………
13. TAARIFA ZA WAZAZI:-
    i. WAPO WOTE………………………………………………………………
    ii. YUPO MMOJA (TAJA- BABA/MAMA)………………………..
    iii. WOTE WAMEFARIKI……………………………………(Weka alamayavema (√)panapohitajika)

Nakirikuwamaelezoyaliyopohapojuunisahihi.

**…………………………………………………….** **……………………………………**

**SAHIHI YA MWANAFUNZI** **SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi (Jina la mwanafunzi)…………………………………………………………………………nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga katika shule hii. Na ahidi kufuata sheria za shule na taratibu zote zilizotolewa na zitakazotolewa na uongozi wa shule.

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi (jina kamili) ……………………………………………………………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………………………nimeyasoma masharti na sheria za shule ya sekondari MANGA ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu

kufuata sheria na taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia mwema wataifa letu.

**TAREHE……………………………………………….…………**
**SAINI YA MWANAFUNZI……………………………….…….**
**JINA LA MWANAFUNZI…………………………………..**

**TAREHE………………………………..……………………….**
**SAINI YA MZAZI/MLEZI……………………………..……..**
**JINA LA MZAZI/MLEZI………………………………………**

# TARIME DISTRICT COUNCIL

**MANGA SEKONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 305**
**TARIME**
**DATE:………………………**

**TO MEDICAL OFFICER**

**………………………………………………**

**………………………………………………**

**………………………………………………**

**Ref:……………………………………………………………………………………………(name of student)**

**Please examine the above named student as per medical examination form.**

**HEADMISTRESS**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**(To be completed by Government medical officer)**

**Full name…………………………………………………………………………………………**

**Age …………………………………Height…………………………………(Cm) Weight……………………(Kg)**

1. **Blood examination……………………………………………………………………………**
2. **Stool examination……………………………………………………………………………**
3. **Urinalysis (Pregnancy) for female………………………………………………………**
4. **Tuberculosis Test (TB) & Leprosy test…………………………………………………**
5. **Eye……………………………………………………………………………………………**
6. **Ear test ……………………………………………………………………………………**
7. **Chest…………………………………………………………………………………………**
8. **Abdomen……………………………………………………………………………………**
9. **Asthma………………………………………………………………………………………**
10. **Spleen………………………………………………………………………………………**
11. **Any chronic complains noted above…………………………………………………**

**Any addition information:**

**E.g.physical defects or impairments,chronics or family diseases like sickle sell, Inabilty to eat certain food e.t.c……………………………………………………………………………………**

**I have examined the named above and consider that he/ she is physically FIT /NOT FIT to pursue secondary education.**

**……………………………………………………………… ………………………………………………**

**Signature and Officer Stamp Date**

**Station ……………………………………… Designation…………………………………**